

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI**

Simu: +255 26 2324455

FAX: +255 26 2323233

Barua pepe: ps@mow.go.tz

Tovuti: www.mow.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,

S.L.P. 2888,

40470 DODOMA.

TANZANIA

DODOMA

17 Januari, 2024

TAARIFA KWA UMMA

Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent Bashungwa (Mb), amezielekeza Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB) na Bodi ya Usajili ya Wakandarasi (CRB) kufika haraka kwenye mradi wa barabara ya Kanyinabushwa – Mbale A Wilayani Misenyi, Mkoani Kagera na kumchukulia hatua stahiki kwa mujibu wa sheria mkandarasi na msimamizi wa ujenzi wa mradi huo kutokana na ujenzi wa makalavati katika barabara hiyo kutozingatia viwango.

Waziri Bashungwa amezielekeza Bodi hizo kufuatia video inayosambaa mitandaoni ikiwaonesha wananchi wakilalamika kuhusu ujenzi wa barabara hiyo kutozingatia viwango.

Waziri Bashungwa ametoa onyo kali kwa Wakandarasi na Wasimamizi wanaojenga na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya barabara chini ya kiwango hali inayosababisha miundombinu hiyo kuharibika mapema na kuhatarisha maisha ya watumiaji wa barabara.

Aidha, Waziri Bashungwa ameleeza kuwa miradi illiyotekelizwa na inayoendelea kutekelezwa inatumia fedha nyingi za watanzania hivyo kitendo cha Wakandarasi kujenga chini ya kiwango kunatiletea hasara kubwa Serikali.

Waziri Bashungwa ametoa wito kwa Wakandarasi wote nchini kuhakikisha wanajenga miundombinu ya barabara kwa kuzingatia viwango kwa mujibu wa mikataba.

Imetolewa na;

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,

Wizara ya Ujenzi